**UJUMBE WA SIKU YA VIWANGO AFRIKA UMEWASILISHWA NA MKURUGENZI MKUU TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS) KATIKA MAADHIMISHO YA SABA (7) YA SIKU YA VIWANGO AFRIKA, TAREHE 21 MACHI, 2019 KATIKA UKUMBI WA SHEIKH IDRISS ABDULWAKIL**

**KAULI MBIU: JUKUMU LA VIWANGO KATIKA KUSHINDA VITA DHIDI YA RUSHWA KWA MABADILIKO ENDELEVU YA AFRIKA**

## 1. UTANGULIZI

Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) imeanzishwa kwa Sheria ya Viwango ya Zanzibar Na. 1 ya mwaka 2011. Kazi za ZBS zimeanza kutekelezwa rasmi mwaka 2012/2013. ZBS inatekeleza majukumu yake chini ya Wizara ya Biashara na Viwanda.

Dhamira kuu ya kuanzishwa ZBS ni kuandaa viwango vya Zanzibar pamoja na kuvisimamia viwango hivyo. Hivyo bidhaa zitakazokaguliwa na ZBS ni lazima zipimwe kwa kuzingatia viwango hivyo kwa ukamilifu wake. Lengo la kuthibitisha ubora wa bidhaa hizo ni kuhakikisha kuwa zinakua salama na kulinda afya ya watumiaji pamoja na mazingira ya nchi. Aidha, kuwepo kwa viwango vya bidhaa na huduma na utekelezaji wa viwango hivyo kunachochea ukuaji wa uchumi kupitia uzalishaji wa bidhaa zenye ubora na biashara ya kimataifa.

Hivyo, ZBS inaungana na wadau wengine katika kuweka mihimili ya ukuaji na uimarikaji wa uchumi wa taifa.

ZBS ni Mwananchama Mwangalizi wa Shirika la Viwango Afrika kufuatia azimio la Mkutano wa 54 wa Baraza na kuidhinishwa rasmi kupitia Mkutano Mkuu wa 22 wa ARSO Juni 2016.

Shirika la Viwango Afrika (ARSO) limeanzishwa miaka 41 iliyopita kwa mashirikiano ya Umoja wa Afrika (AU) na Kamisheni ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa Afrika (UNECA) kwa madhumuni ya kusimamia ajenda ya uendelezaji wa viwango kwa maendeleo endelevu ya Afrika pamoja na

kuweka fursa za kujenga uwelewa juu ya changamoto zinazoibuka ikiwemo suala la rushwa.

## 2. Ujumbe Katika Kuadhimisha Siku ya Viwango Afrika

Siku ya Viwango Afrika inaadhimishwa kwa mwaka wa saba (7) na kwa mara ya kwanza ZBS inaadhimisha siku hiyo baada ya miaka miwili tokea ilipopata uanachama wa ARSO.

Kauli mbiu ya Siku ya Viwango Afrika katika maadhimisho haya ya saba (7) ni **"JUKUMU LA VIWANGO KATIKA KUSHINDA VITA DHIDI YA RUSHWA KWA MABADILIKO ENDELEVU YA AFRIKA"** inaendana na azma ya kuanzishwa kwa ARSO.

Mkutano wa Baraza la ARSO uliofanyika Nairobi Kenya tarehe 6 Disemba 2018 umeweka azimio kuwa Siku ya Viwango Afrika iadhimishwe tarehe 21 Machi ya kila mwaka, ikiwa ni kuweka kumbukumbu ya kusainiwa makubaliano ya kuwa "Bara la Afrika ni Eneo Huru la Biashara" (African Continental Free Trade Area (AfCFTA) Agreement). Utekelezaji wa Afrika kuwa ni eneo huru la biashara kwa nchi wanachama, ni mradi wa kipaumbele wa ajenda ya Umoja wa Afrika hadi mwaka 2063. Makubaliano hayo yalisainiwa Kigali katika Jamhuri ya Rwanda tarehe 21 Machi 2018 katika Mkutano Mkuu wa Kilele wa Dharura wa Wakuu wa nchi za Umoja wa Afrika.

Eneo Huru la Biashara Barani Afrika limeweka kipaumbele katika kuongeza thamani bidhaa na huduma zinazozalishwa Afrika "Made in Africa" kwa ajili ya kuongeza ukuaji wa biashara ndani ya Bara la Afrika kwa asilimia 52.3 kwa kuondosha kodi za uagiziaji na kuongeza ukuaji huo wa biashara maradufu iwapo vikwazo visivyokuwa vya kodi navyo vitapungua hususan vikwazo vya kiufundi katika biashara (TBTs), pamoja na kuwa na bidhaa mbadala za uagiziaji kupitia bidhaa zinazotengenezwa Afrika.

Nchi za Afrika ni lazima zijidhatiti katika kujenga uelewa juu ya madhara ya rushwa. Katika kazi za uendelezaji viwango, ni vyema kauli mbiu hii ya Siku ya Viwango Afrika ikafahamika vyema katika mazingira ya kuendelea kushamiri kwa bidhaa bandia katika Afrika na madhara yake katika uzalishaji na bidhaa zinazozalishwa Afrika katika kushajihisha biashara ndani ya Afrika na kuongeza ushindani wa kibishara.

Tunaadhimisha Siku ya Viwango Afrika kwa mwaka huu wa 2019 ikiwa ni pamoja na kujenga uelewa wa Kiwango cha Afrika kilichochapishwa hivi karibuni cha "Matumizi Mazuri ya Fedha za Misaada" (ARS 1651:2018). Kiwango hicho mbali ya kuwa kinatumika na wadau katika Afrika kimevutia wadau wengine katika mabara mengine duniani. Kiwango hicho kinatoa sura, njia za kuweka usawa, kurahisisha na kuimarisha usimamizi wa fedha za misaada kwa muda wote wa kutolewa msaada huo kwa manufaa ya mtoaji na anayepewa msaada huo.

Shirika la Viwango Afrika, linatoa wito kwa wanachama ikiwemo Zanzibar kutekeleza Kiwango cha Kimataifa cha "Mifumo ya Usimamizi dhidi Utoaji Hongo" - ("Anti-bribery Management Systems" - ISO 37001:2016).

Rushwa husababisha matokeo mabaya na kudhoofisha utulivu wa kisiasa, kuongeza gharama katika uendeshaji wa biashara na kuchangia kuongezeka kwa umaskini. Kwa maana hiyo rushwa huleta madhara makubwa ya kiuchumi.

Kwa mujibu wa Benki ya Dunia zaidi ya Dola za Kimarekani trilioni moja za hongo zinatoka mkono mmoja kwenda mkono mwengine kila mwaka. Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa, fedha zinazopotea kutokana na rushwa zinakisiwa kuwa ni mara kumi zaidi ya fedha zinazotolewa kama misaada ya maendeleo kwa nchi za Afrika. Hali hiyo inaweza kuwa ni kikwazo cha kufikiwa kwa Maendeleo Endelevu (SDGs) katika nchi za Afrika ifikapo mwaka 2030.

Zanzibar ikiwa ni sehemu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Afrika ni lazima tujidhatiti katika kujenga uelewa juu ya madhara ya rushwa. Katika tasnia ya viwango ni vyema tukaifahamu vyema **Kauli Mbiu ya Jukumu la Viwango katika vita dhidi ya rushwa kwa mabadiliko endelevu barani Afrika** kwa kupata fursa na kuweko na dhima ya kupambana dhidi ya rushwa na kuondosha mazingira yatakayotoa mwanya wa rushwa. Fursa hizo zinazoweza kupatikana kupitia viwango ni pamoja na kuziba mianya na kuondosha vichocheo vya kikanuni vinavyoweza kupelekea utoaji wa rushwa, kuhakikisha taratibu nzuri za usimamizi wa ndani kwa mujibu wa vipengele vinavyowekwa katika viwango husika. Uandaaji wa viwango unaozingatia kanuni na taratibu nzuri za kimataifa huondoa mianya ya rushwa. Kwa mfano kanuni na taratibu za uandaaji wa viwango zinapofuatwa ipasavyo huhakikisha utabiri mzuri, uwazi katika taasisi na utawala wa sheria ikiwa ni pamoja na manunuzi na usimamizi wa fedha. Viwango huelezea kitu gani kinaweza au hakiwezi kubadilishana na chengine na hivyo huondosha fursa za vitendo vya rushwa.

Kuadhimisha Siku ya Viwango Afrika kunatupa fursa ya kuelimishana juu ya madhara ya rushwa katika kufikia Afrika kuwa ni Eneo Huru la Biashara na namna ya utekelezaji wa viwango unavyopelekea kuwa na miundombinu au taasisi za kusimamia Ubora (quality infrastructure) zinavyoweza kutoa fursa ya mapambano dhidi ya rushwa.

**HITIMISHO**

Zanzibar ikiwa ni mwanachama mwangalizi wa Shirika la Viwango Afrika kupitia Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) itaendelea kushirikiana na wazalishaji wa ndani wa bidhaa na huduma kupitia kuongeza thamani na kuweka misingi imara ya mashirikiano. Kwa kufanya hivyo, Zanzibar itaweza kushiriki vyema katika uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa zenye ubora kwa kuzingatia viwango na kuleta ushindani ndani ya Eneo Huru la Biashara la Afrika.

**AHSANTENI**